MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA (NHIF)

JARIDA LA MTANDAONI

ISO 9001:2015 CERTIFIED



BIMA YA AFYA KWA WOTE, SASA NI KWA KILA MTANZANIA

Mtwara



Bima Ya Afya Kwa Wote— Tuwashe Mshumaa, Tuwashe Tanzania - Mchengerwa

Afya ni hitaji muhimu ambapo uwezo wa kifedha haupaswi kuwa kikwazo cha kupata matibabu. Kwa kulitambua hilo, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imezindua Awamu ya Pili ya Utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo uliofanyika kitaifa Oktoba 22, 2026 katika Uwanja wa Sabasaba, mkoani Mtwara,, Waziri wa Afya, Mhe. Mohamed Mchengerwa, alieleza kuwa mpango huu unalenga kupunguza mzigo mkubwa wa gharama za matibabu kwa wananchi, huku Serikali ikigharamia wasio na uwezo.

Pia Mhe. Mchengerwa alisema, katika Awamu ya Kwanza, kaya 198,709 kati ya 276,004 zilizolengwa (sawa na asilimia 72) zilihakikiwa na kupewa kadi, huku Mkoa wa Mtwara ukiongoza kitaifa. Katika Awamu ya Pili, Serikali imejipanga kusajili kaya 625,000, zikiwemo za wakulima, wafugaji, wavuvi, wafanyabiashara, madereva wa bodaboda, mama lishe, na wafanyakazi wa sekta binafsi, kupitia vifurushi nafuu kama vile Fahari Afya kwa Shilingi laki moja na nusu kwa mwaka kwa kaya ya watu sita.

Aidha sambamba na Mkoa wa Mtwara ambako ndko yalipokuwa makao makuu ya uzinduzi, pia uzinduzi huo ulifanyika katika mikoa mingine ya Tanzania Bara ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Njombe, Pwani, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida, Songwe, Tabora, na Tanga. Wananchi wanahimizwa kuchagua vifurushi sahihi kulingana na uwezo wao na kutumia kadi hizo kwa uaminifu ili kufanikisha azma hii.





Arusha



Arusha Yaanza Awamu ya Pili ya Bima ya Afya Kwa Wote, Kaya 111 Zakabidhiwa Vitambulisho

Mkoa wa Arusha umeanza rasmi utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote kupitia uzinduzi uliofanyika Oktoba 22, 2026, katika viwanja vya Field Force, Kata ya Muriet, jijini Arusha ambapo jumla ya Kaya 111 zisizo na uwezo zilikabidhiwa vitambulisho vya matibabu.

Uzinduzi huo ulijumuisha ugawaji wa vitambulisho kwa kaya zisizo na uwezo, uhamasishaji wa wananchi kujiunga na kifurushi cha Fahari Afya na utoaji wa huduma za uchunguzi wa afya bila malipo.

Aidha tukio hilo lilikwenda sambamba na upimaji wa afya bure, ambapo jumla ya wananchi 272 walipatiwa huduma za vipimo mbalimbali kupitia watoa huduma walioshiriki tukio hilo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, CPA Gabriel Makalla, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Mhe. Neema K. Lugangira, aliwataka watendaji wa Mkoa, Halmashauri na NHIF kuanza mara moja usajili wa kaya zisizo na uwezo lakini pia kuhamasisha wananchi kutumia fursa hiyo kujiunga na bima ya afya kupitia kifurushi cha Fahari Afya.

Alisisitiza umuhimu wa vituo vya kutolea huduma kuwa na dawa, vifaa tiba na watumishi wanaotoa huduma kwa weledi na lugha nzuri kwa wateja.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Dkt. Toba Nguvila, alieleza kuwa hadi wakati wa uzinduzi, Mkoa ulikuwa umekabidhi vitambulisho kwa kaya 7,416 kati ya kaya 12,673 zilizolengwa katika awamu iliyotangulia, sawa na asilimia 58.8.

Kwa upande wake, Meneja wa NHIF Mkoa wa Arusha, Hipoliti Lello, aliishukuru Serikali ya Mkoa na kuzipongeza Halmashauri za Jiji la Arusha, Longido na Meru kwa hatua zilizopiga katika zoezi hilo. Alizihimiza Halmashauri nyingine kuongeza juhudi ili kufikia lengo la kusajili kaya 29,334 katika Awamu ya Pili.

Akielezea kifurushi cha Fahari Afya alisema kinapatikana kwa mchango wa Shilingi 150,000 kwa mwaka kwa kaya yenye wanufaika wasiozidi sita, sawa na wastani wa Shilingi 25,000 kwa mnufaika mmoja kwa mwaka.

Uzinduzi huo umeweka msisitizo katika kuongeza usajili, kupanua uelewa wa wananchi na kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kwa makundi mbalimbali ya jamii.

Pwani



Jiungeni na Bima ya Afya Kwa Wote- RC Pwani

Mkoa wa Pwani umeendelea kuhamasisha wananchi kutumia fursa ya Bima ya Afya kwa Wote kupitia uzinduzi wa Awamu ya Pili ya mpango huo, uliohusisha viongozi wa Serikali, wataalamu wa afya na wananchi kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhe. Stanslaus Nyongo, alisisitiza umuhimu wa wananchi kujiunga na bima ya afya ili kupunguza mzigo wa gharama za matibabu na kuimarisha ustawi wa familia.

Alieleza kuwa Serikali inaendelea kuweka mikakati ya kuboresha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na wataalamu wa afya katika vituo vya kutolea huduma, ili wananchi watakaojiunga na mpango huo wapate huduma zinazostahili.

Sambamba na uzinduzi, wananchi walipata elimu kuhusu umuhimu wa bima ya afya na fursa za kujiunga na mpango huo. Pia, huduma za upimaji wa afya bila malipo zilitolewa, zikiwemo uchunguzi wa magonjwa yasiyoambukiza kama shinikizo la damu na kisukari.

Uzinduzi huo umetoa fursa kwa wananchi kupata taarifa kuhusu bima ya afya na umuhimu wa kujikinga dhidi ya gharama za matibabu huku Serikali, NHIF na wadau wengine wakiendelea na mikakati ya kuwafikia wananchi.





Manyara



Manyara Yajipanga Kusajili Kaya Zaidi ya 43,000 Katika Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote

Mkoa wa Manyara umezindua Awamu ya Pili ya usajili wa Bima ya Afya kwa Wote katika Kijiji cha Naberera, Wilaya ya Simanjiro, Oktoba 22, 2026, huku ukiweka malengo ya kusajili kaya zisizo na uwezo na kaya zenye uwezo wa kuchangia ili kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za afya.

Uzinduzi huo uliongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Mhe. Martin Shigella, ambaye alizielekeza Halmashauri kuweka mikakati madhubuti ya usajili na kuwataka watoa huduma kuboresha huduma za afya ili kukidhi mahitaji ya wananchi watakaojiunga na mpango huo.

Katika Awamu ya Pili, Mkoa wa Manyara unalenga kusajili kaya 23,090 zisizo na uwezo, zenye wanufaika 61,702, pamoja na kaya 20,000 zenye uwezo wa kuchangia, ambazo zinalingana na asilimia tano ya kaya zote za Mkoa kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022.

Wakati wa uzinduzi, kaya 24 zikiwemo kaya zisizo na uwezo zilisajiliwa katika Kijiji cha Naberera na kupewa vitambulisho vya matibabu.

Aidha, wananchi 123 walipata fursa ya kupima afya bure ambapo vipimo hivyo vilijumuisha shinikizo la damu, sukari, malaria, homa ya ini, VVU, uzito, urefu na uwiano wa uzito na urefu (BMI).



Mkuu wa Mkoa alisisitiza kuwa mafanikio ya mpango huo yanategemea ushiriki wa wananchi, usimamizi wa Halmashauri na uwepo wa huduma bora katika vituo vya afya.

Uzinduzi huo umeweka msingi wa kuendeleza usajili katika maeneo mbalimbali ya Manyara, kwa lengo la kuhakikisha kaya zinazostahili zinapata fursa ya kujumuishwa katika mfumo wa bima ya afya.



Kigoma



Kigoma Yasajili Kaya 156 Katika Uzinduzi wa Awamu ya Pili ya Bima ya Afya Kwa Wote

Mkoa wa Kigoma umeanza utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote kwa kusajili kaya 156 zenye wanufaika 310, katika uzinduzi uliofanyika Oktoba 22, 2026, eneo la Rusimbi, Manispaa ya Kigoma.

Uzinduzi huo uliongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, IGP Mstaafu Mhe. Balozi Simon Nyakoro Sirro, na ulihusisha viongozi wa Mkoa na Halmashauri, watumishi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), wadau mbalimbali na wananchi.

Katika tukio hilo, takribani wananchi 1,500 walikadiriwa kufika na kupata elimu kuhusu umuhimu wa bima ya afya, taratibu za kujiunga na namna ya kutumia huduma zinazotolewa kupitia bima.

Elimu hiyo ililenga kuongeza uelewa



wa wananchi kuhusu umuhimu wa kujikinga dhidi ya gharama za matibabu na kuimarisha ushiriki wao katika mpango huo.

Katika hatua nyingine, kaya 156 zenye wanufaika 310 zilisajiliwa na kupatiwa vitambulisho vya huduma huku taarifa za wanachama wa kikundi cha Kigoma Football Club zikichukuliwa kwa ajili mchakato wa usajili kupitia kifurushi cha Faraja Afya.

Sambamba na shughuli za usajili na elimu, jumla ya wananchi 148 walijitokeza kupima afya zao wakati wa uzinduzi huo.

Uzinduzi huo umeendelea kufungua fursa kwa wananchi wa Kigoma kupata elimu na kujiunga na bima ya afya, huku ushirikiano kati ya Serikali, NHIF na wadau ukiendelea kuwa muhimu katika kuongeza idadi ya wanufaika na kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za afya.



Jiungeni na Bima ya Afya Kwa Wote Kabla ya Kuugua - RC Iringa

Mkoa wa Iringa umeanza utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote kwa kusisitiza uwajibikaji wa viongozi na ushiriki wa wadau katika kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanajiunga na mpango huo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Mhe. Kheri James, alieleza dhamira ya Serikali ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya kwa wakati bila kubebeshwa mzigo mkubwa wa gharama za matibabu. Aliwahimiza wananchi kujiunga na bima ya afya mapema badala ya kusubiri hadi wanapougua.

Katika uzinduzi huo, wananchi 102 walitembelea banda la NHIF kwa ajili ya kupata elimu kuhusu vifurushi mbalimbali vya bima ya afya. Kati yao, kaya 26 zisizo na uwezo zilisajiliwa na wanufaika 33 walipatiwa kadi wakati wa tukio hilo.

Aidha, wananchi 68 walipatiwa huduma za uchunguzi wa afya, zikiwemo huduma za macho, kinywa na meno, pamoja na uchunguzi wa magonjwa yasiyoambukiza kwa kupima shinikizo la damu, sukari, uzito na urefu.

Ili kuhakikisha utekelezaji wa mpango huo unakuwa na matokeo chanya, Mkuu wa Mkoa alizitaka Halmashauri kufanya vikao na watendaji wa kata, vijiji na mitaa kwa lengo la kuweka mikakati ya uhamasishaji na utekelezaji. Wakuu wa Wilaya walitakiwa kuratibu vikao na viongozi wa vijiji na mitaa, huku madiwani wakihamasisha wananchi katika maeneo yao.

Aidha, waajiri wa sekta binafsi na taasisi za umma walihimizwa kuhakikisha wafanyakazi wao wanakuwa na bima ya afya kwa kuzingatia sheria na taratibu husika. Sekretarieti ya Mkoa na Wakuu wa Wilaya walitakiwa kusimamia utekelezaji huo.

Kwa upande wake, NHIF Mkoa wa Iringa imeagizwa kuendelea kutoa elimu, ufafanuzi wa masuala ya bima na usaidizi wa kitaalamu kwa viongozi na wadau. Maelekezo hayo yanaweka msisitizo katika kuimarisha uhamasishaji kuanzia ngazi ya Mkoa hadi vijijini na mitaani, ili kuongeza uelewa na ushiriki wa wananchi katika Bima ya Afya kwa Wote.

Tanga



Tanga Yaelimisha Wananchi 725, Wengine 546 Wapimwa Afya Katika Uzinduzi wa Bima ya Afya kwa Wote

Mkoa wa Tanga umeendelea kuimarisha uhamasishaji wa wananchi kujiunga na Bima ya Afya kwa Wote kupitia uzinduzi wa Awamu ya Pili uliofanyika Oktoba 22, 2026, katika viwanja vya Ofisi ya Kijiji cha Mkata Mashariki, Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

Katika uzinduzi huo, Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Mhe. Salum Nyamwese, alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dkt. Batilda Salha Burian Mwakilishi huyo alitoa maelekezo kwa watendaji wa Serikali katika ngazi za Mkoa, Wilaya na Halmashauri kuhusu umuhimu wa kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya kutosha juu ya faida, umuhimu na utaratibu wa kujiunga na bima ya afya.

Alisisitiza pia usimamizi wa usajili katika kata, vijiji na mitaa yote, pamoja na kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya vinakuwa na dawa, vifaa tiba na huduma muhimu zinazohitajika kuwahudumia wanachama.

Katika shughuli zilizoambatana na uzinduzi, wananchi 546 walipatiwa huduma za uchunguzi wa afya bila malipo. Kati yao, wananchi 471 walipimwa shinikizo la damu na sukari ya damu, watu 25 walipimwa macho, huku watu 50 wakipatiwa uchunguzi wa saratani ya matiti na elimu kuhusu ugonjwa huo.

Kwa upande wa usajili, kaya 35 zenye wanufaika 48 zilijiunga na kifurushi cha Fahari Afya. Aidha, vikundi sita vyenye wanufaika 57 vilisajiliwa kupitia kifurushi cha Umoja Afya.

Uzinduzi huo pia ulitoa fursa ya kuelimisha wananchi 725 kuhusu Bima ya Afya kwa Wote na namna ya kunufaika na huduma zinazopatikana kupitia mpango huo.

Mgeni rasmi alisisitiza kuwa mafanikio ya mpango huo yanahitaji ushirikiano, uwajibikaji na dhamira ya dhati kutoka kwa kila mtendaji na mdau. Alieleza umuhimu wa kuhakikisha hakuna mwananchi anayeachwa nyuma katika jitihada za kupanua upatikanaji wa huduma za afya.

Matokeo ya uzinduzi huo yanaonesha mchango wa elimu kwa umma, usajili na huduma za uchunguzi wa afya katika kuimarisha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote mkoani Tanga.



JARIDA LA MTANDAONI

Kagera Kusajili Kaya 38,217 Bima Ya Afya Kwa Wote

Mkoa wa Kagera umeweka lengo la kusajili kaya 38,217 zenye jumla ya wanufaika 84,934 katika Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Uzinduzi wa awamu hiyo ulifanyika katika viwanja vya Shule ya Msingi Kashai, Manispaa ya Bukoba, ukiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Kanali Yahya Kido.

Akizungumza katika hafla hiyo, Kanali Kido alieleza kuwa mpango huo unalenga kuwafikia wananchi wa makundi mbalimbali, yakiwemo kaya zenye uhitaji, vikundi vya kijamii na vyama vya ushirika.

Alibainisha kuwa kaya maskini zinazotambuliwa rasmi zitasajiliwa kwa gharama za Serikali, hatua



inayolenga kupunguza mzigo wa gharama za matibabu kwa wananchi wenye kipato cha chini.

Kwa upande wa kaya zenye uwezo wa kuchangia, Mkuu wa Mkoa alieleza kuwa kifurushi husika kinapatikana kwa Shilingi 150,000 kwa mwaka kwa kaya yenye wanufaika wasiozidi sita.

Aidha, aliwaagiza Wakurugenzi wa Halmashauri kwa kushirikiana na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kuhakikisha mifumo ya utambuzi na usajili inafika hadi vijijini na mitaani ili wananchi wote wanaostahili wapate fursa ya kujiunga.

Uzinduzi huo unaashiria hatua muhimu katika juhudi za Mkoa wa Kagera za kuongeza usajili wa kaya na kuimarisha uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa bima ya afya. Utekelezaji wake unatarajiwa kusaidia kupanua upatikanaji wa huduma za matibabu na kupunguza athari za kifedha zinazotokana na gharama za matibabu.



Dar Es Salaam Yatambua Wadau 24 Katika Uzinduzi wa Awamu ya Pili ya Bima ya Afya Kwa Wote

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Albert John Chalamila, amewahimiza wananchi kujiunga na bima ya afya kupitia kifurushi cha Fahari Afya ili kuongeza uwezo wa kaya kupata huduma za matibabu na kupunguza athari za gharama za matibabu katika maisha ya kila siku.

Rai hiyo aliitoa wakati wa uzinduzi wa Awamu ya Pili ya utekelezaji wa Bima ya Afya kwa wote Mkoa wa Dar es Salaam uliofanyika Oktoba 22, 2026, katika viwanja vya Mnazi Mmoja.

Alisema kuwa kifurushi cha Fahari Afya kinapatikana kwa Shilingi 150,000 kwa mwaka kwa kaya yenye wanufaika wasiozidi sita, hivyo kutoa fursa kwa wananchi kujiandaa kukabiliana na mahitaji ya matibabu.

Katika hafla hiyo, tuzo zilitolewa kwa viongozi wa Mkoa, wakiwemo Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa na viongozi wa Manispaa, kwa kutambua mchango wao katika kuunga mkono utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa Wote.

Aidha, Mfuko ulitoa vyeti vya utambuzi vilitolewa kwa wadau 24, wakiwemo waajiri watatu, vyuo sita, shule sita na watoa huduma za afya tisa, ikiwa ni ishara ya kutambua ushiriki wao katika kuendeleza huduma za afya na utekelezaji wa mpango huo.

Uzinduzi huo pia ulihusisha ushuhuda wa wanufaika waliosajiliwa kupitia utaratibu wa kaya zisizo na uwezo, ambao walieleza uzoefu wao wa kupata huduma za afya kupitia NHIF.

Uzinduzi huo pia ulihusisha utoaji wa huduma za uchunguzi wa afya bila malipo kwa lengo la kuwasaidia wananchi kutambua hali ya afya zao.

Kwa ujumla, uzinduzi huo uliimarisha uhamasishaji wa wananchi kuhusu fursa za kujiunga na Fahari Afya na kutambua mchango wa wadau katika kufanikisha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote. Takwimu za jumla za wananchi waliosajiliwa na waliopimwa afya hazikutajwa katika taarifa iliyowasilishwa.



Uzinduzi Awamu ya Pili Bima ya Afya Kwa Wote Yachochea Elimu Dodoma

Mkoa wa Dodoma umezindua rasmi Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote Oktoba 22, 2026, katika Soko la Wazi la Machinga, Kata ya Majengo, Jiji la Dodoma, kwa lengo la kuongeza uelewa wa wananchi na kupanua usajili wa wanufaika.

Mgeni rasmi katika uzinduzi huo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Mhe. Alhaj Jabir Shekimweri, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule.

Katika hafla hiyo, wananchi walipatiwa elimu kuhusu umuhimu wa bima ya afya, utaratibu wa kujiunga na namna ya kutumia bima kupata huduma za matibabu.

Uzinduzi huo ulipata mwitikio mkubwa wa wananchi ambapo takribani wananchi 500 walishiriki



ambao walipatiwa elimu kuhusu umuhimu na huduma za bima ya afya ambapo jumla ya wananchi 69 walisajiliwa.

Aidha jumla ya wananchi 272 walipatiwa huduma za uchunguzi wa afya na ushauri wa kitaalamu bila malipo. Huduma hizo zilitolewa kwa ushirikiano na Hospitali ya Benjamin Mkapa, Taasisi ya Afya ya Akili Tanzania, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma, DCMC-T Ntyuka, Hospitali ya St. Camillus, Mwangaza Polyclinic na JM Solomon Polyclinic.

Ushiriki wa vituo hivyo uliwezesha wananchi kupata huduma za uchunguzi wa afya katika eneo la tukio, huku ukiimarisha ushirikiano kati ya NHIF na watoa huduma za afya.

Uzinduzi huo umeonesha umuhimu wa kutumia maeneo yenye mikusanyiko ya wananchi, hususan masoko, kufikisha elimu ya bima ya afya na kusogeza huduma za uchunguzi karibu na jamii.



Wananchi Njombe Waitikia Usajili Bima ya Afya Kwa Wote

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) Mkoa wa Njombe umeandikisha wanachama 91 katika uzinduzi wa Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote uliofanyika Oktoba 22, 2026, katika viwanja vya Stendi ya Zamani.

Uzinduzi huo uliongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Njombe Mjini, Mhe. Juma Sweda, na ulihusisha shughuli za uelimishaji, uandikishaji wa wanachama, upimaji wa afya na uchangiaji wa damu.

Wadau mbalimbali walishiriki katika tukio hilo, wakiwemo waajiri, watoa huduma za afya na vyama vya ujasiriamali, kwa lengo la kuhamasisha wananchi kutumia fursa zinazotolewa kupitia bima ya afya.



Wananchi waliojisajili walijiunga kupitia kifurushi cha Fahari Afya na Umoja Afya hatua hii inayoonesha mwitikio wa wananchi na makundi mbalimbali katika kutumia fursa za kujiunga na bima ya afya.

Sambamba na shughuli za usajili, upimaji wa afya na uchangiaji wa damu vilitoa nafasi ya kuunganisha uhamasishaji wa bima ya afya na huduma zinazochangia ustawi wa jamii.

Uzinduzi huo umeendelea kuimarisha juhudi za NHIF Mkoa wa Njombe za kufikisha elimu kwa wananchi, kuhamasisha usajili na kushirikiana na wadau katika kupanua upatikanaji wa huduma za afya kupitia Bima ya Afya kwa Wote.

Geita



Vituo 326 Vya Kutolea Huduma za Matibabu Geita Kuhudumia Wananchi Kupitia Bima ya Afya Kwa Wote

Mbunge Geita aahidi kugharamia kaya 200

Mkoa wa Geita umeendelea na juhudi za kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi kupitia uzinduzi wa Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote uliofanyika tarehe 22 Oktoba 2026 katika Viwanja vya CCM Katoro. Uzinduzi huo uliongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Geita, Mhe. Alexander Mnyeti, ukiwa na lengo la kuhamasisha wananchi kujiunga na bima ya afya na kujikinga dhidi ya gharama za matibabu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mhe. Mnyeti alisisitiza umuhimu wa wananchi kuwa na bima ya afya ili kupunguza mzigo wa gharama za matibabu na kulinda ustawi wa familia zao. Aliwahimiza wananchi kutumia fursa inayotolewa na mpango huo ili waweze kupata huduma za afya kwa utaratibu wa bima.

Kwa upande wake, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Geita, Dkt. Omari Sukari, alieleza kuwa mkoa huo una vituo 326 vya kutolea huduma za afya vilivyo tayari kutoa huduma kwa wananchi kupitia mpango huo. Utayari wa vituo hivyo ni hatua muhimu katika kusaidia utekelezaji wa mpango na kupanua upatikanaji wa huduma za afya.

Katika kuunga mkono juhudi hizo, Mbunge wa Jimbo la Geita, Mhe. Joseph Msukuma, aliahidi kugharamia bima ya afya kwa kaya 200, ikiwa ni sehemu ya mchango wake katika kuhakikisha wananchi wanapata ulinzi wa afya na kurahisishiwa upatikanaji wa huduma za matibabu.

Uzinduzi huo pia uliambatana na utoaji wa elimu kuhusu Bima ya Afya kwa Wote na huduma za upimaji wa afya. Takribani wananchi 1,300 walikadiriwa kufika na kupata elimu kuhusu mpango huo, huku zaidi ya wananchi 200 wakijitokeza kupima afya zao.

Mafanikio yaliyopatikana katika uzinduzi huo yanaonesha umuhimu wa ushirikiano kati ya Serikali, viongozi, NHIF na wadau wengine katika kuhamasisha wananchi kujiunga na bima ya afya. Hatua inayofuata ni kuendeleza elimu kwa wananchi na kuhakikisha huduma zinatolewa kwa ubora na kwa wakati kulingana na stahiki za wanufaika.

Mbeya



Mbeya Wahamasishwa Kujiunga na Bima ya Afya Kwa Wote

Halmashauri zilizofanya vizuri uandikishaji wa kaya zatambuliwa

Mkoa wa Mbeya umeendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na Bima ya Afya kwa Wote kupitia uzinduzi wa Awamu ya Pili ya utekelezaji wa mpango huo uliofanyika katika Viwanja vya Kata ya Isanga, Jijini Mbeya.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Mhe. Jumanne Abdallah Sagini, wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, wananchi na wadau mbalimbali wa sekta ya afya.

Katika hotuba yake, Mhe. Sagini aliwataka wananchi kuchangamkia fursa ya Bima ya Afya kwa Wote kwa kujiunga na mpango huo ili kupata ulinzi wa kifedha dhidi ya gharama za matibabu na kurahisisha upatikanaji wa huduma za afya wanapozihitaji.
Aidha, aliwaelekeza Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha kuwa mpango huo unatekelezwa kikamilifu katika maeneo yao ya kiutawala. Alisisitiza kuwa usimamizi wa utekelezaji utazingatia matokeo ya uandikishaji wa wananchi katika maeneo husika, akiwataka viongozi kuweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanafikiwa.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Mkoa wa Mbeya una wakazi 2,343,754, wakiwemo wanaume 1,123,828 na wanawake 1,219,929. Idadi hiyo inaonesha umuhimu wa kuendelea kuimarisha elimu na uhamasishaji ili wananchi wengi zaidi waweze kunufaika na mfumo wa bima ya afya.

Shughuli zilizofanyika wakati wa uzinduzi zilijumuisha upimaji wa afya bila malipo, utoaji wa elimu kuhusu umuhimu wa kuwa na bima ya afya na ugawaji wa kadi kwa wanufaika waliokamilisha taratibu za usajili.

Aidha, NHIF ilitambua mchango wa wadau mbalimbali waliotoa huduma bora za bima ya afya kwa kuwapatia vyeti. Halmashauri tatu zilizofanya vizuri zaidi katika uandikishaji wa kaya za wananchi wasio na uwezo wa kumudu gharama za bima ya afya katika Awamu ya Kwanza nazo zilitambuliwa na kutunukiwa vyeti.

Utambuzi huo ni sehemu ya kuhamasisha ushindani chanya na kuongeza uwajibikaji miongoni mwa wadau wanaoshiriki katika utekelezaji wa mpango huo.

Uzinduzi wa Awamu ya Pili mkoani Mbeya umeweka msisitizo katika kuimarisha uelewa wa wananchi, kuongeza uandikishaji na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya. Ushirikiano kati ya Serikali, NHIF, Halmashauri, wadau na wananchi utaendelea kuwa muhimu katika kufanikisha malengo ya Bima ya Afya kwa Wote.



Kaya 87 Zapatiwa Kadi za Bima ya Afya, Zaidi ya Wananchi 122 Wapimwa

Mkoa walenga kusajili kaya 22,024 katika Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote

Mkoa wa Simiyu umeanza utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote kwa kusajili kaya za wananchi wasio na uwezo wa kumudu gharama za bima na kuanzisha rasmi usajili wa wananchi kupitia kifurushi cha Fahari Afya. Uzinduzi huo ulifanyika tarehe 22 Oktoba 2026 katika Viwanja vya Wazi vya Somanda, vilivyopo mkabala na Stendi na Soko la Somanda, Kata ya Somanda, Wilaya ya Bariadi.

Katika uzinduzi huo, kaya 87 za wananchi wasio na uwezo zilisajiliwa na kukabidhiwa kadi za bima ya afya, huku kaya sita zikisajiliwa kupitia kifurushi cha Fahari Afya. Aidha, wananchi zaidi ya 122 walipata huduma za upimaji wa afya bila malipo kupitia vituo viwili vya kutolea huduma vilivyoshiriki katika shughuli hiyo.

Mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Mhe. Simon P. Simalenga, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Mhe. Said M. Mtanda. Katika hotuba yake, aliwataka watendaji kuanzia ngazi ya Mkoa hadi vijiji na mitaa kuhakikisha kuwa mpango huo unatekelezwa kwa ufanisi na kuwafikia wananchi wote bila kuacha makundi nyuma.

Alisisitiza umuhimu wa kutumia lugha rahisi katika kutoa elimu kwa wananchi, kushirikisha viongozi wa dini, wazee, watu maarufu na wahudumu wa afya, pamoja na kuboresha ubora wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya. Pia alielekeza kuimarishwa kwa mifumo ya usajili, uhakiki wa wanufaika na uwasilishaji pamoja na ulipaji wa madai.

Kwa upande wa maandalizi ya huduma, Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Simiyu, Dkt. Yudas Ndungile, alieleza kuwa mkoa una zaidi ya vituo 253 vya kutolea huduma za afya. Kati ya hivyo, zaidi ya asilimia 94 vimejiunga na kuanza kutumia mfumo wa GoTHOMIS, huku zaidi ya asilimia 90 vikiwa vimeunganisha mifumo yao na mifumo ya NHIF.

Alieleza kuwa mkoa unalenga kuhakikisha vituo vyote vinatumia mifumo ya kielektroniki kwa asilimia 100 ili kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma, uhakiki wa wanufaika na uwasilishaji wa madai.

Naye Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji wa NHIF, Bw. Celestine Muganga, aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Dkt. Irene Isaka, alisisitiza umuhimu wa kutumia mifumo ya kielektroniki katika kutambua na kuhakiki wanufaika kabla ya kupata huduma. Alieleza kuwa NHIF imeboresha mifumo yake ya TEHAMA ili kuwezesha uwasilishaji, uchakataji na ulipaji wa madai kwa ufanisi na kwa wakati.

Katika Awamu ya Kwanza, Mkoa wa Simiyu ulisajili kaya 11,223, sawa na asilimia 77.5 ya lengo lililowekwa. Kwa Awamu ya Pili, mkoa umeweka lengo la kusajili kaya 22,024, hivyo Halmashauri na wadau wametakiwa kuongeza juhudi za uelimishaji na uandikishaji.

Aidha, Halmashauri za Mji wa Bariadi, Wilaya ya Bariadi na Itilima zilipongezwa kwa kufanya vizuri zaidi katika uandikishaji wa kaya za wananchi wasio na uwezo katika awamu iliyopita.

Wananchi wenye uwezo wa kuchangia walihamasishwa kujiunga kupitia kifurushi cha Fahari Afya, kinachopatikana kwa shilingi 150,000 kwa mwaka kwa kaya yenye wanufaika wasiozidi sita, kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa wakati wa uzinduzi.

Mafanikio ya utekelezaji wa mpango huo mkoani Simiyu yataendelea kutegemea ushirikiano kati ya Serikali, NHIF, Halmashauri, TASAF, wataalamu wa afya na wadau wengine, pamoja na matumizi ya mifumo ya kielektroniki na utoaji wa huduma bora kwa wanufaika.



Viongozi Wawekewa Msisitizo wa Kusimamia Uandikishaji wa Bima ya Afya kwa Wote

Uzinduzi wa Awamu ya Pili waambatana na elimu, upimaji wa afya na ugawaji wa kadi

Mkoa wa Singida umeimarisha maandalizi ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote kwa kuwajengea viongozi na wadau uelewa kuhusu majukumu yao katika kuhamasisha wananchi kujiunga na mpango huo. Uzinduzi huo ulifanyika tarehe 22 Oktoba 2026 chini ya uongozi wa Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Singida, Mhe. Godwin Gondwe.

Shughuli za uzinduzi zilifanyika katika sehemu mbili kuu: kikao cha ndani cha maelekezo kwa viongozi na wadau wa utekelezaji, pamoja na uzinduzi rasmi katika viwanja vya Kituo cha Afya Sokoine.

Kikao cha ndani kilishirikisha Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Sekretarieti ya Mkoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, viongozi wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wa mkoa na wilaya, waratibu wa bima ya afya, waratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), viongozi wa dini na wazee maarufu.

Lengo la kikao hicho lilikuwa kuimarisha uelewa wa viongozi na watendaji kuhusu utekelezaji wa mpango na kuweka wazi wajibu wa kila mdau katika kutoa elimu na kuongeza idadi ya wananchi wanaojiandikisha.

Akizungumza katika kikao hicho, Kaimu Mkuu wa Mkoa aliwaelekeza Wakuu wa Wilaya kuunda kamati zitakazosimamia na kuratibu shughuli za usajili wa wananchi katika Bima ya Afya kwa Wote. Pia aliwataka kuhakikisha kila wilaya inaandaa na kutekeleza uzinduzi rasmi wa mpango huo ili kuongeza uelewa na kuhamasisha ushiriki wa wananchi katika maeneo yao.
Baada ya kikao hicho, uzinduzi rasmi ulifanyika katika viwanja vya Kituo cha Afya Sokoine. Wananchi waliohudhuria walipatiwa elimu kuhusu umuhimu wa kuwa na bima ya afya, faida za kujiunga, taratibu za usajili na namna ya kupata huduma katika vituo vilivyosajiliwa vinavyohudumia wanachama wa bima ya afya.

Uzinduzi huo pia uliambatana na huduma za upimaji wa afya, zilizowapa washiriki fursa ya kufahamu hali zao za afya na kuhamasishwa kujenga utamaduni wa kupima afya mara kwa mara. Aidha, kadi za bima ya afya zilikabidhiwa kwa wananchi waliojiunga na kukamilisha taratibu zinazohitajika.

Katika kutambua mchango wa wadau, tuzo na vyeti vilitolewa kwa wale walioonesha mchango mzuri katika kusaidia na kuunga mkono utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote. Hatua hiyo ililenga kuwatia moyo wadau hao na kuhamasisha wengine kushiriki kikamilifu katika kufanikisha mpango.

Uzinduzi wa Awamu ya Pili mkoani Singida umeweka msingi wa kuimarisha ushirikiano kati ya viongozi, watendaji, wadau na wananchi. Utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa, kuendelea kutoa elimu na kusimamia shughuli za usajili ni miongoni mwa hatua muhimu za kuhakikisha mpango unawafikia wananchi wengi zaidi na kuchangia upatikanaji wa huduma za afya kupitia mfumo wa bima.



Tumeitikia Wito wa Dkt. Samia Kuhusu Bima ya Afya, Kaya 3,900 Zasajiliwa Awamu ya Kwanza – RC Malima

Mkoa wa Lindi umefanikiwa kusajili kaya 3,900 kati ya kaya 4,793 zilizolengwa katika awamu ya kwanza ya mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, sawa na asilimia 81 ya lengo. Kaya hizo zina jumla ya wanufaika takribani 10,500 ambao wameanza kunufaika na huduma za afya kupitia mpango huo.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Usajili wa Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote mkoani Lindi, Mkuu wa Mkoa huo, Adam Malima, amesema mafanikio hayo ni hatua muhimu katika kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma za afya, huku akihimiza kuimarishwa kwa uhamasishaji na ufuatiliaji wa kaya ambazo bado hazijasajiliwa.

Aidha, amewataka viongozi wa serikali za mitaa na wadau kuendelea kutoa elimu sahihi kuhusu mpango huo, huku waganga wakuu na wasimamizi wa vituo vya kutolea



huduma za afya wakihakikisha wanufaika wanapokelewa vizuri na kupata huduma stahiki. Pia, amesisitiza changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa mpango huo kuripotiwa na kutatuliwa kwa wakati.

Kwa upande wake, Meneja wa NHIF Mkoa wa Lindi, Ridhia Makono, amesema katika awamu ya pili mkoa huo unalenga kusajili kaya 19,821 zenye jumla ya wanufaika 37,411. Amesema mpango huo unalenga kuwezesha wananchi kutoka kaya zisizo na uwezo kupata huduma za afya kupitia bima na kupunguza changamoto za kugharamia matibabu.

Aidha, RC Malima amezihimiza halmashauri, NHIF na vituo vya kutolea huduma za afya kuimarisha ushirikiano ili kuhakikisha wananchi waliosajiliwa wanapata huduma bora kwa wakati na changamoto zinazoweza kuathiri upatikanaji wa huduma hizo zinatatuliwa kwa pamoja.

Mwanza



Mwanza Yaweka Msisitizo Katika Utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote

CP Salum Hamduni ataka usajili wenye ufanisi, huduma bora na usimamizi madhubuti

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa CP Salum Hamduni, amesisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya viongozi wa Serikali, Halmashauri, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na wadau wengine katika kuhakikisha utekelezaji wa awamu ya pili ya Bima ya Afya kwa Wote unaleta matokeo chanya kwa wananchi.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa awamu hiyo uliofanyika Oktoba 22, 2026, katika Ukumbi wa Mahatma Ghand, Wilaya ya Nyamagana, alieleza kuwa mafanikio ya mpango huo yatategemea usimamizi madhubuti, elimu kwa umma na uwezo wa kuhakikisha wananchi wanapata huduma za afya wanazostahili.

Alibainisha kuwa Bima ya Afya kwa Wote ni nyenzo muhimu ya kulinda familia dhidi ya athari za kifedha zinazotokana na gharama za matibabu, huku ikiwasaidia wananchi kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na kijamii.

Alieleza kuwa utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya mwaka 2023 ni hatua muhimu katika kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za bima ya afya nchini, sambamba na juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuboresha huduma za afya.

Katika kusimamia utekelezaji wa mpango huo, Mkuu wa Mkoa alizielekeza Halmashauri zote kuimarisha uratibu na kuweka mikakati madhubuti ya kuwafikia wananchi katika maeneo yao ya shughuli za kila siku. Alisisitiza umuhimu wa kutoa elimu katika masoko, maeneo ya uvuvi, vituo vya bodaboda, maeneo ya kilimo na vikundi vya kiuchumi ili kuhakikisha wakulima, wavuvi, wafanyabiashara wadogo, vijana, wazee na makundi mengine wanaelewa umuhimu wa kujiunga na bima ya afya na taratibu za kupata huduma.

Aidha, alielekeza Halmashauri kushirikiana na TASAF pamoja na viongozi wa maeneo husika katika kutambua na kuhakiki kaya zinazostahili kusaidiwa na Serikali kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Vilevile, aliwataka wataalamu wa afya na NHIF kuhakikisha vituo vya kutolea huduma za afya vilivyoingia mikataba vina dawa, vifaa tiba na mifumo inayowezesha wanachama kupata huduma kwa mujibu wa mafao na masharti ya bima zao. Alisisitiza kuwa malalamiko ya wananchi yanapaswa kushughulikiwa kwa wakati ili kuimarisha ubora wa huduma na imani ya wananchi katika mfumo wa bima ya afya.

Akizungumzia uwajibikaji, Mheshimiwa Hamduni alielekeza kufanyika kwa ufuatiliaji na tathmini za mara kwa mara katika ngazi za Mkoa, Wilaya na Halmashauri ili kupima maendeleo ya usajili, utayari wa vituo vya afya, upatikanaji wa dawa na namna changamoto zinavyotatuliwa. Pia alisisitiza usimamizi sahihi wa rasilimali, uadilifu katika uwasilishaji wa madai ya huduma na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kurahisisha usajili na utoaji wa huduma. Alibainisha kuwa mafanikio ya mpango huo hayapaswi kupimwa kwa idadi ya wananchi walioandikishwa pekee, bali pia kwa ubora wa huduma wanazopata.

Katika kuhitimisha hotuba yake, Mkuu wa Mkoa aliipongeza NHIF kwa kufikisha miaka 25 ya utekelezaji wa majukumu yake, akieleza kuwa uzoefu wa Mfuko huo ni msingi muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote.

Uzinduzi huo uliambatana na zoezi la upimaji afya bure kwa wananchi ambapo zaidi ya wananchi 200 walipima afya zao.

Songwe



Songwe Yazindua Awamu ya Pili Ya Bima ya Afya kwa Wote, Kaya 6 za Wasio na Uwezo Zapatiwa Vitambulisho

Wananchi 112 wanufaika na upimaji wa afya bure, huku Mkoa ukilenga kusajili kaya 9,922 katika awamu hii

Mkoa wa Songwe umezindua awamu ya pili ya utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, ikiwa ni sehemu ya juhudi za Serikali za kupanua wigo wa wananchi wanaopata huduma za afya na kuhakikisha kaya zenye uhitaji zinapata fursa ya kunufaika na huduma hizo. Uzinduzi huo ulifanyika Oktoba 22, 2026, katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma, ukiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Mheshimiwa Abubakari Mussa Kunenge.

Katika uzinduzi huo, vitambulisho vya bima ya afya viligawiwa kwa kaya sita za wananchi wasio na uwezo kutoka Kata za Mpemba na Chapwa. Aidha, kaya tatu zilisajiliwa kupitia kifurushi cha Fahari Afya, huku wananchi 112 wakipatiwa huduma za uchunguzi wa afya bila malipo kupitia Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Songwe (Songwe RRH) na Hospitali ya Mji wa Tunduma. Hatua hizo zililenga kuhamasisha wananchi kujiunga na bima ya afya na kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa kujikinga dhidi ya gharama za matibabu.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkuu wa Mkoa, Mheshimiwa Abubakari Mussa Kunenge, aliwaelekeza watendaji kuhakikisha usajili wa wananchi wasio na uwezo unakamilishwa ndani ya siku 14. Pia alisisitiza umuhimu wa kuimarisha elimu na uhamasishaji kwa wananchi wanaofanya shughuli katika sekta isiyo rasmi ili waweze kujiunga na kifurushi cha Fahari Afya na kunufaika na huduma za bima ya afya.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Mkoa wa Songwe, Dkt. Frank George Haule, alieleza kuwa Mkoa ulikuwa umeshagawa vitambulisho kwa kaya 3,881 kati ya kaya 4,864 zilizolengwa, sawa na asilimia 82.2. Alibainisha kuwa hatua hiyo inaonesha maendeleo yaliyofikiwa katika kuwafikia kaya zinazostahili, huku jitihada zikiendelea kuhakikisha kaya zilizobaki zinakamilishiwa taratibu za kupata vitambulisho.

Naye Meneja wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) alizipongeza Halmashauri za Momba, Ileje na Mbozi kwa kuongoza kimkoa katika utekelezaji wa shughuli za bima ya afya. Alieleza kuwa Mkoa wa Songwe umejiwekea lengo la kusajili kaya 9,922 katika awamu hii na kuwakumbusha wananchi kuwa kifurushi cha Fahari Afya kinagharimu shilingi 150,000 kwa mwaka kwa kaya yenye wanufaika wasiozidi sita, sawa na wastani wa shilingi 25,000 kwa mtu mmoja kwa mwaka.

Uzinduzi huo unaonesha umuhimu wa ushirikiano kati ya Serikali za Mitaa, NHIF na vituo vya kutolea huduma za afya katika kuimarisha usajili, kutoa elimu na kusogeza huduma karibu na wananchi. Kupitia hatua hizo, Mkoa wa Songwe unaendelea kuhamasisha makundi mbalimbali, hususan wananchi wa sekta isiyo rasmi na kaya zenye uhitaji, kushiriki katika mpango wa Bima ya Afya kwa Wote ili kuongeza fursa ya kupata huduma za afya na kupunguza athari za kifedha zinazotokana na maradhi.



Ongezeni Kasi ya Elimu Bima ya Afya Kwa Wote- RC Mara

Ataka usajili ufanyika kwa asilimia 100

Mkuu wa Mkoa wa Mara, Brigedia Jenerali Evans Mtambi, amezindua rasmi Awamu ya Pili ya utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote mkoani Mara, akisisitiza umuhimu wa kuongeza kasi ya utoaji wa elimu na usajili wa wananchi ili kuhakikisha kila mwananchi anapata fursa ya kunufaika na huduma za afya.

Uzinduzi huo uliofanyika katika Manispaa ya Musoma ni sehemu ya juhudi za Serikali za kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya kwa wakati na kupunguza changamoto za gharama za matibabu, hususan kwa kaya zenye uhitaji, makundi maalumu, vikundi vya ushirika na jamii kwa ujumla.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Brigedia Jenerali Mtambi aliwaagiza Wakuu wa Wilaya kwa kushirikiana na Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha elimu kuhusu Bima ya Afya kwa Wote inatolewa kwa wananchi na usajili unafanyika nyumba kwa nyumba ili kufikia lengo la asilimia 100 ya usajili wa wanufaika wanaostahili.
Alieleza kuwa kiwango cha usajili kilichofikiwa na Mkoa wa Mara katika awamu ya kwanza kilikuwa cha chini ikilinganishwa na mikoa mingine, hivyo akataka changamoto zilizosababisha kutofikiwa kwa malengo zichunguzwe na kupatiwa ufumbuzi ili kuboresha utekelezaji katika awamu hii ya pili.

Aidha, Mkuu huyo wa Mkoa alisisitiza kuwa Bima ya Afya kwa Wote ni mpango muhimu wa kuwakomboa wananchi dhidi ya changamoto za kumudu gharama za matibabu, hivyo alielekeza suala hilo liwe ajenda ya kudumu katika vikao vya Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) na Kamati za Ushauri za Wilaya (DCC) kwa ajili ya kufuatilia maendeleo ya elimu, usajili na utoaji wa huduma.

NHIF YAENDELEA NA USAJILI NA ELIMU KWA WANANCHI

Katika shughuli za uzinduzi huo, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) uliendesha shughuli za uhakiki na usajili wa wanufaika wa kaya zisizo na uwezo, ambapo kaya nane (8) zilisajiliwa na kupewa kadi za Bima ya Afya. Aidha, mwananchi mmoja (1) alijitokeza kwa ajili ya kusajiliwa katika mpango huo, huku wananchi 71 wakihudumiwa kupitia dawati la Mfuko.

WANANCHI WANUFAIKA NA UPIMAJI WA AFYA BURE

Sambamba na uzinduzi huo, wananchi walipata huduma za upimaji wa afya kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere na Hospitali ya Manispaa ya Musoma.

Huduma zilizotolewa zilihusisha upimaji wa macho, afya ya kinywa na meno, uchunguzi wa moyo kwa kutumia kipimo cha ECHO, Ultrasound, uchunguzi wa magonjwa yasiyoambukiza pamoja na huduma za lishe.

Utoaji wa huduma hizo ni sehemu ya jitihada za kuhamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kupima afya mara kwa mara, kutambua changamoto za kiafya mapema na kuchukua hatua stahiki za kupata matibabu.

Kupitia Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote, Mkoa wa Mara unatarajiwa kuongeza juhudi za uhamasishaji, usajili na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mpango huo ili wananchi wengi zaidi wanufaike na huduma za afya na kufikia lengo la Serikali la kuhakikisha huduma za afya zinapatikana kwa wote.

Morogoro



Suala la Bima ya Afya kwa Wote ni la Wote- RC Morogoro

Asisitiza kuwafikia wananchi na kuwasajili

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Queen Cuthbert Sendiga, amezindua rasmi Awamu ya Pili ya utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote mkoani humo, akisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa viongozi na wadau katika kuhakikisha wananchi wengi zaidi wananufaika na huduma za afya kupitia mfumo wa bima.

Uzinduzi huo uliofanyika tarehe 23 Oktoba 2026 katika Manispaa ya Morogoro ulihudhuriwa na Katibu Tawala wa Mkoa, Wakuu wa Wilaya na Makatibu Tawala wa Wilaya zote saba, Kaimu Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Wakurugenzi wa Halmashauri zote tisa, Waganga Wakuu wa Halmashauri, Waratibu wa Bima ya Afya, wakuu wa taasisi, wadau mbalimbali pamoja na wananchi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhe. Sendiga alisisitiza umuhimu wa kuipa kipaumbele ajenda ya Bima ya Afya kwa Wote katika ngazi za mkoa na wilaya ili kuongeza kasi ya uhamasishaji na usajili wa wananchi. Aliwaelekeza viongozi wa wilaya kuhakikisha suala hilo linajadiliwa katika vikao vyao hadi lengo la kuwafikia wananchi wote wanaostahili kunufaika na mpango huo litakapofikiwa.

Aidha, alieleza kuwa Serikali inaendelea kuimarisha miundombinu ya afya, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba ili kuhakikisha ongezeko la wananchi wanaojiunga na bima linaenda sambamba na utoaji wa huduma bora na za uhakika.

WADAU WA NHIF WATAMBULIWA KWA MCHANGO WAO

Katika uzinduzi huo, wadau mbalimbali wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoani Morogoro walitunukiwa tuzo za kutambua mchango wao katika usajili wa wanachama, utoaji wa huduma bora na uzingatiaji wa taratibu na kanuni zinazosimamia huduma za bima ya afya.
Utoaji wa tuzo hizo ni sehemu ya kutambua ushirikiano wa wadau katika kutekeleza majukumu ya Mfuko na kuhamasisha mwendelezo wa utoaji wa huduma zenye ubora, ufanisi na zinazozingatia mahitaji ya wanachama.
Ushirikiano kati ya NHIF, viongozi wa Serikali, vituo vya kutolea huduma za afya na wadau wengine ni muhimu katika kuhakikisha wananchi wanapata elimu sahihi kuhusu bima ya afya na wanahudumiwa kwa mujibu wa stahiki zao.

USAJILI WA WANACHAMA NA UPIMAJI WA AFYA BILA MALIPO

Sambamba na uzinduzi huo, wananchi waliohudhuria walipata fursa ya kujisajili katika Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote na kupata elimu kuhusu umuhimu wa kuwa na bima ya afya kwa ajili ya kukabiliana na gharama za matibabu wanapougua.

Aidha, wananchi walipata huduma za upimaji wa afya bila malipo, hatua iliyolenga kuhamasisha jamii kujenga utamaduni wa kuchunguza afya zao na kutambua mapema changamoto mbalimbali za kiafya.

Huduma hizo ziliifanya hafla ya uzinduzi kuwa jukwaa la kuunganisha elimu ya bima ya afya, usajili wa wanachama na uhamasishaji kuhusu umuhimu wa kujikinga na athari za kifedha zinazoweza kusababishwa na gharama za matibabu.
Kupitia uzinduzi wa awamu hii ya pili, Mkoa wa Morogoro unaendelea kuhamasisha ushiriki wa wananchi na wadau katika kufanikisha azma ya Serikali ya kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za afya, kupunguza vikwazo vya kifedha na kuimarisha ustawi wa jamii.
Mafanikio ya mpango huo yanategemea ushirikiano wa karibu kati ya viongozi, watoa huduma za afya, wasimamizi wa bima na wananchi wenyewe ili kuhakikisha usajili unaongezeka na huduma zinazotolewa kwa wanachama zinakuwa bora, za uhakika na zinazozingatia haki za wanufaika.



Wananchi Jiungeni Bima ya Afya kwa Wote- RC Tabora

Mkoa wa Tabora umezindua rasmi Awamu ya Pili ya utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote tarehe 22 Oktoba 2026, katika Manispaa ya Tabora, kwa lengo la kuongeza wigo wa wananchi wanaopata huduma za afya kupitia bima na kupunguza changamoto za kifedha zinazoweza kuwazuia kupata matibabu wanapoyahitaji.

Uzinduzi huo uliongozwa na Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Mhe. Gerald Romuald Mongella, ukihudhuriwa na Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Katibu Tawala wa Mkoa, Kaimu Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Wakurugenzi wa Halmashauri zote nane pamoja na wadau mbalimbali wa sekta ya afya.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mhe. Mongella alisisitiza umuhimu wa wananchi kujiunga na bima ya afya ili kujikinga dhidi ya gharama kubwa za matibabu na kuimarisha ustawi wa familia. Aliwataka viongozi na watendaji wa Serikali kushirikiana na wadau katika kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kujisajili, hususan katika maeneo yao ya shughuli za kiuchumi na kijamii.

Alieleza kuwa maeneo ya masoko, vituo vya bodaboda, shughuli za kilimo na vikundi vya kiuchumi ni miongoni mwa maeneo muhimu ya kuwafikia wananchi kwa ajili ya utoaji wa elimu na kuratibu usajili wa wanachama.

Kwa upande wake Meneja wa NHIF Mkoa wa Tabora, Dkt. Raphael Malaba, alihimiza wananchi kujitokeza kujiunga na mpango huo ili kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha.

WADAU WATUNUKIWA TUZO KUTAMBUA MCHANGO WAO

Katika hafla hiyo, wadau mbalimbali wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoani Tabora walitunukiwa tuzo kama ishara ya kutambua mchango wao katika kuboresha huduma, kuzingatia taratibu na kanuni na kushiriki katika utekelezaji wa majukumu ya Mfuko.
Tuzo hizo ni sehemu ya kuhamasisha wadau kuendelea kutoa huduma zenye ubora, kuimarisha uwajibikaji na kujenga ushirikiano unaolenga kuboresha uzoefu wa wanachama wanapopata huduma za afya.

Ushirikiano wa wadau ni muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, kwa kuwa mpango huu unahitaji uratibu wa karibu kati ya Serikali, NHIF, watoa huduma za afya na wananchi ili kuhakikisha elimu sahihi inawafikia walengwa na huduma zinapatikana kwa mujibu wa mafao na masharti ya bima.

TABORA KUWAFIKIA WANANCHI WENGI ZAIDI KUPITIA USAJILI

Katika Awamu ya Pili Mkoa wa Taobora unalenga kusajili kaya 23,773 zenye jumla ya wanufaika 57,129.

Takwimu hizo zinaonesha ukubwa wa kazi inayopaswa kufanyika katika kuongeza uelewa wa wananchi, kuwafikia walengwa na kuratibu usajili ili kaya nyingi zaidi ziweze kupata ulinzi wa kifedha dhidi ya gharama za matibabu.

Kwa upande wake, Katibu Tawala wa Mkoa wa Tabora, Dkt. John Mboya, alieleza kuwa changamoto zilizojitokeza katika awamu ya kwanza zimekuwa fursa ya kujifunza na kuboresha utekelezaji wa awamu ya pili, huku akibainisha kuwa Mkoa umejiandaa kuendelea na juhudi za kuutekeleza mpango huo.



Kilimanjaro Yazindua Awamu Ya Pili Ya Bima Ya Afya Kwa Wote

Yajipanga Kupanua Wigo wa Wanachama

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mhe. Nurudini Babu, amezindua rasmi Awamu ya Pili ya utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote mkoani humo, tarehe 22 Oktoba 2026, katika Manispaa ya Moshi, ikiwa ni sehemu ya juhudi za Serikali za kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za afya na kupunguza changamoto za kifedha zinazoweza kuwazuia wananchi kupata matibabu wanapoyahitaji.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, Wakuu wa Wilaya, Katibu Tawala wa Mkoa, Waganga Wakuu wa Wilaya, Waratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), viongozi wa dini, Kaimu Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Wakurugenzi wa Halmashauri zote saba pamoja na wadau mbalimbali wa sekta ya afya.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhe. Babu alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya viongozi wa Serikali, wataalamu wa afya na wadau wengine katika kuhakikisha wananchi wanapata elimu kuhusu umuhimu wa bima ya afya na kushiriki kikamilifu katika mpango huo.
Alieleza kuwa kuimarisha uelewa wa wananchi kuhusu bima ya afya ni hatua muhimu katika kupunguza athari za gharama za matibabu kwa familia na kuwapa fursa ya kupata huduma za afya wanapozihitaji.

USAJILI WA WANANCHI KUWA KIPAUMBELE

Awamu ya Pili ya Bima ya Afya kwa Wote inalenga kupanua wigo wa usajili kwa kuwafikia wananchi wa makundi mbalimbali, wakiwemo wakulima, wafugaji, wafanyabiashara, wavuvi, madereva wa bodaboda, mama lishe na wananchi wengine wanaojishughulisha na shughuli za sekta isiyo rasmi.
Kwa Mkoa wa Kilimanjaro, ushiriki wa viongozi wa mkoa na wilaya, Halmashauri, waratibu wa TASAF na wadau wa sekta ya afya ni muhimu katika kuwafikia wananchi wanaostahili kunufaika na mpango huo, kutoa elimu sahihi na kuratibu shughuli za usajili.

Ushirikiano huo pia unatoa fursa ya kubaini changamoto zinazoweza kuathiri usajili na upatikanaji wa huduma, ili ziweze kushughulikiwa kwa wakati na kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa mpango.

NHIF YATAMBUA MCHANGO WA WADAU KATIKA UTOAJI WA HUDUMA BORA

Katika hafla hiyo, wadau mbalimbali wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoani Kilimanjaro walitunukiwa tuzo kwa kutambua mchango wao katika utoaji wa huduma bora na uzingatiaji wa taratibu na kanuni zinazosimamia huduma za bima ya afya.

Tuzo hizo zinalenga kuthamini mchango wa wadau katika kuboresha huduma kwa wanachama na kuhamasisha uwajibikaji, weledi na ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yanayohusiana na bima ya afya.

Ushirikiano wa wadau una umuhimu mkubwa katika kuhakikisha kuwa wananchi wanaojiunga na bima wanapata huduma kwa mujibu wa stahiki zao. Hili linahitaji kuimarisha usajili, utoaji wa taarifa sahihi kwa wanachama na usimamizi wa ubora wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya.

UBORA WA HUDUMA NA UPATIKANAJI WA DAWA NI NGUZO MUHIMU

Katika utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, Serikali imesisitiza umuhimu wa kuhakikisha upanuzi wa usajili unaenda sambamba na upatikanaji wa huduma bora, dawa na vifaa tiba.



Shinyanga Yazindua Rasmi Bima ya Afya kwa Wote Awamu ya Pili

Uzinduzi wa Bima ya Afya kwa Wote Awamu ya Pili umefanyika rasmi mkoani Shinyanga tarehe 22 Oktoba 2026, ukiwa ni sehemu ya juhudi za Serikali za kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi na kupunguza vikwazo vya kifedha vinavyoweza kuwazuia kupata matibabu wanapoyahitaji.

Uzinduzi huo umefanyika katika Manispaa ya Shinyanga ukiongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Mhe. Mboni Mhita, akiongozana na viongozi mbalimbali wa Serikali na wadau wa maendeleo. Miongoni mwa viongozi walioshiriki ni Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, Wakuu wa Wilaya na Makatibu Tawala, pamoja na Kaimu Mwenyekiti wa CCM Mkoa, Wakurugenzi wa Halmashauri zote sita za Mkoa wa Shinyanga na Wakuu wa Taasisi mbalimbali.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkuu wa Mkoa alisisitiza umuhimu wa Bima ya Afya kwa Wote katika kuwezesha wananchi kupata huduma za matibabu kwa wakati bila kukabiliwa na changamoto kubwa za kifedha. Aidha, alieleza umuhimu wa ushirikiano kati ya Serikali, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), watoa huduma za afya na wadau wengine katika kuhamasisha wananchi kuelewa na kutumia fursa zinazotolewa na mpango huo.



Bima ya Afya kwa Wote inalenga kupanua wigo wa wananchi wanaonufaika na huduma za afya kupitia mifumo ya bima, kwa kuzingatia umuhimu wa ulinzi wa kifedha dhidi ya gharama za matibabu. Utekelezaji wa mpango huo unatarajiwa kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya na kuchangia ustawi wa wananchi, hususan makundi yenye uhitaji mkubwa wa huduma hizo.

Katika hafla hiyo, wadau mbalimbali wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya mkoani Shinyanga walitunukiwa tuzo za kutambua mchango wao katika utoaji wa huduma bora na uzingatiaji wa taratibu na kanuni zinazosimamia huduma za bima ya afya. Tuzo hizo ni sehemu ya kutambua ushirikiano na juhudi zinazofanywa na wadau katika kuboresha huduma kwa wanachama na kuimarisha imani ya wananchi kwa mfumo wa bima ya afya.

Aidha, ushiriki wa viongozi wa Serikali, taasisi na wadau mbalimbali katika uzinduzi huo unaonesha umuhimu wa ushirikiano wa pamoja katika kuhamasisha wananchi kujiunga na bima ya afya na kuongeza uelewa kuhusu manufaa yake. Uhamasishaji wa wananchi unatarajiwa kusaidia kufikia makundi mbalimbali katika jamii na kuhakikisha kuwa taarifa sahihi kuhusu mpango huo zinawafikia walengwa.

Uzinduzi wa Bima ya Afya kwa Wote Awamu ya Pili mkoani Shinyanga ni hatua muhimu katika kuendeleza jitihada za kupanua upatikanaji wa huduma za afya na kuimarisha ulinzi wa kifedha kwa wananchi. Kupitia ushirikiano wa Serikali, NHIF, watoa huduma za afya na wadau wengine, wananchi wanahimizwa kupata taarifa sahihi kuhusu mpango huo na kuchukua hatua zinazofaa ili kunufaika na huduma za afya kupitia mifumo ya bima.